watoto waliochini ya miaka 16 kisiwani Pemba.

Kamati imeitaka Mahakama kuweka jitihada kwa watoto ambao hawajafikia umri wa miaka 16 ambao hawatakiwi kupelekwa chuo cha Mafunzo kwa kuharakisha ujenzi wa Chuo cha Mafunzo kwa watoto wanaokinzana na Sheria kwa upande wa Pemba.

*(d)* Kamati imependekeza Wizara kulichukulia hatua za haraka suala la upatikanaji wa Hatimiliki ya jengo na eneo la Mahakama Kuu, Tunguu.

Kamati inasisitiza kutafuta hatimiliki ya viwanja hivyo ili kuepusha migogoro ya mipaka yanayoweza kutokea hapo baadae hasa kutokana na kuwa maeneo hayo yamekuwa yanauhamiaji mkubwa wa watu hivi sasa.

*(e)* Kamati imeelezwa kuwepo mpango wa kufanyiwa ukarabati kwa jengo la Afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka walilopatiwa na Serikali katika Mahakama ya Wete.

Kamati imeishauri ofisi ya DPP kufanya tathmini upya ya ukarabari wa jengo la afisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka Wilaya ya Wete, jengo ambalo wamepatiwa na Serikali kwa ajili ya kulifanyia ukarabati kwa matumizi yao. Aidha, Kamati imeona ni vyema kufikiria kujenga upya kuliko kufanya ukarabati wa jengo hili ambalo ni kongwe mno na halikidhi vigezo vya Ofisi ya Mwendesha Mashtaka.

*(f)* Kamati inaishauri Kamisheni ya Wakfu na Mali ya Amana kushirikiana na Ofisi ya Mufti Mkuu wa Zanzibar kutoa elimu ya mirathi kupitia miskiti hasa katika hotuba za Ijumaa.

Kamati imetoa msisitizo kwa Wizara kuhakikisha kuwa inaishajihisha jamii juu ya kutoa elimu hiyo kwakuwa tatizo la mirathi limekuwa endelevu katika jamii zetu na husababisha mpaka vifo visivyokusudiwa.

